

Ukweli wa Injili

Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa
Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote

BWANA, TUFUNDISHE KUOMBA

(Katika sehemu hii ya jalida tumenukuu Ombi la Bwana kutoka kitabu cha Mathayo 6:9-13 SUV)

Katika Luka 11 Wanafunzi wa Kristo walimwendea wakiwa na ombi: “Bwana, tufundishe jinsi ya kuomba.” Ombi walilopewa lilikuja kufanyika ombi kuu zaidi kati ya maombi yote ambayo yashawahi kuandikwa: “Ombi la Bwana,” na ni mfano bora wa kuigwa. Litakuwa jambo la baraka kubwa ikiwa tutajifunza kutoka kwa Mwana wa Mungu jinsi tunastahili kuomba. Ombi hili lina vipengele vingi ambavyo vitawezesha watu kuomba kwa njia ya kuwawezesha kupata majibu ya maombi yao, kulingana na jinsi wanavyofungua mioyo yao kwa dhati na upendo kwa Bwana, huku wakitoka mioyo yao kumwabudu Mungu na kufanya maombi yao: “Basi ninyi salini hivi; . . .”

“Baba Yetu”—Uhusiano wa Kibinafsi.

Mwanzo wa ombi hilo unaonyesha uhusiano wa ajabu ambao unastahili kuwoko kati ya Mungu na wanadamu. Tamko hili linaonyesha mtu mwenye uhakika na Mungu baba yake, na kuonyesha upendo ambao sisi watoto wake tuko nao kwake. Sisi ni waridhi wa Mfalme. Neno “Yetu” linaonyesha wingi, na linaonyesha umoja na kukubali kwamba Mungu (pia) ni Baba wa watoto wengine, ndugu na dada zetu wa kiroho.

“Uliye mbinguni,”—Imani/Kutambua.

Ufahamu wa kweli na wa uhakika kwamba Mungu hupatikana kila mahali kwa wakati mmoja, na pia kwamba Yeye anajua kila kitu. Sisi tunamwamini na kumjua Yeye tunayemwomba.

“Jina lako litukuzwe.”—Kuinua/Kutukuza/Kuabudu.

Neno kutukuza linaonyesha kile ambacho kimetakaswa kwa ajili ya kutumika kwa kazi fulani. Wakati wa maombi ni wakati wa kumheshimu na kumsujudu Mungu na kutambua mioyoni mwetu, akilini

mwetu, na kwa maneno yetu, kwamba Yeye ni Mungu mwenye uungu, mwenye sifa takatifu, na kumpatia heshima zake maishani mwetu. Kamwe hatustahili kuanza maombi kwa kuitisha, bali tunastahili kuanza kwa kuabudu jina takatifu la Mungu.

“Ufalme wako uje.”—Kungojea kwa hamu/Matarajio.

Sehemu hii ndio ya kumwomba Mungu kwa matarajio ya kupata mwongozo na uwepo wake. Sehemu yenyewe inaonyesha shauku la mwombaji, shauku la utawala na usimamizi kamili wa Mungu maishani mwetu, na kuvunjiliwa mbali kwa nguvu za Shetani. “Maana ufalme wa Mungu si kula wala kunywa, bali ni haki na amani na furaha katika Roho Mtakatifu” (Warumi 14:17). Ufalme wa Kristo ni wa kiroho, unapatikana ndani mwetu.

“Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni.”—Kunyenyekea/Kujitoa kwa Mungu.

Mapenzi ya Mungu huwa kamili Mbinguni, lakini katika maisha haya ya mpito mapenzi yake hufanyika kulingana na jinsi tunavyonyenyekea kwa mapenzi na mipango yake. Kama Yesu alivyoomba hapo Gethsemane, “Si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe.” Kusudi moja la maombi ni kusalimisha kwa Mungu yote yaliyomo ndani mwetu, kila kilicho chetu, vyote vitumike na Mungu pekee.

“Utupe leo riziki yetu.”—Maombi/Kufanya Sala.

Baada ya kuabudu na kujitoa kwa Mungu sasa tuko katika hali inayofaa ya kumtafuta Mungu ili atupatie mahitaji ya kila siku. Sasa tuna nafasi ya kumwomba Mungu yote tunayohitaji na hata mahitaji ya maisha ya kiroho ili tuweze kutimiza mapenzi yake maishani. Maombi haya hayahusishi tu mahitaji ya kimwili pekee, bali hata kupata neema za kiroho zitakazotusaidia kukua na kupata nguvu za kukabiliiana na udhaifu wetu.

(Endelea katika Ukurasa 2)



“Ombi walilopewa lilikuja kufanyika ombi kuu zaidi kati ya maombi yote ambayo yashawahi kuandikwa: “Ombi la Bwana,” na ni mfano bora wa kuigwa.”

Tahariri

Mafundisho ya Biblia:
MaombiMafunzo Kuhusu
Maombi

Maswali na Majibu

Je, Wajua?

Neno Linalofaa kwa
Msimu Huu

MAMBO AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA KUHUSU...

Neno la Mungu

2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

Uhusiano wa Upendo

Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

Toba

Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

Uzao Mpya

Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4,
Efe. 2:1, 5-6

Uhuru Kutokana na Dhambi

1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

Ujazo wa Roho Mtakatifu

Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

Utakatifu

Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16,
Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

Ufalme wa Mungu

Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

Kanisa

Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13,
Kol. 1:18

Umoja

Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

Kanuni za Kanisa

Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27,
Yn. 13:14-17

Uponyaji wa Kiungu

Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

Utakatifu wa Ndoa

Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3,
I Kor. 7:10-11

Urembo wa Nje

I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

Mwisho wa Nyakati

2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10,
Mt. 25:31-46

Kupenda Amani

Lk. 6:27-29, 18:20

Ibada

Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

Wajibu Mkuu

Mk. 16:15

(Inaendelea kutoka Ukurasa 1)

“Utusamehe deni zetu”—Kukiri/Kusali. Sisi hatustahili msamaha wa Mungu, lakini Yeye ana shauku na utayari wa kutusamehe, sio dhambi zetu tu, bali pia makosa yetu na upungufu wetu wote. Ni muhimu sisi kujichunguza na kutambua upungufu wetu wa kiroho kwa unyenyekevu mkuu moyoni. Ombi la toba ya msamaha linaweza kufanywa hata na kikundi cha watu, kama Daniel alivyoombea taifa la Israeli ili Mungu awasamehe.

“Kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu.”—Huruma/Msamaha. Mungu yu tayari kutusamehe mradi tu tayari kuwahurumia na kuwarehemu wale wanaotukosea. Msaada wa Mungu katika mahusiano yetu na watu wale wengine ni jambo muhimu kwenye mahusiano yetu na Yeye.

“Na usitutie majaribuni”—Kuongozwa (na Mungu). Majaribu na hali zingine hatari za kiroho ni mambo yanayotukumba. Hata kama tutafuata mwongozo wa Mungu (kwa nia ya kweli) bado tutakumbana na majaribu, lakini haitakuwa lazima tuanguke majaribuni na kutenda dhambi. Kutafuta na kutii mwongozo wa Mungu ni jambo litakalotukinga tusitumbukie kwenye matatizo mengi.

**“Maombi ndio
hutuunganisha
na Mungu na ni
muhimu kabisa
maishani mwa
Mkristo.”**

**“lakini utuokoe na yule mwovu.”—Usalama/
Kumtegemea Mungu.** Nguvu za ushindi hazipatikani ndani yetu bali katika nguvu za Mungu. Yeye ndiye atakayetulinda dhidi ya hadaa na mitego ya adui kama tutadumu tukimtegemea ili atupatie msaada wa kila siku.

“Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu”—Kumtambua (Mungu). Sisi ni viumbe dhaifu ambavyo hatuwezi kujitoshesha, lakini ndani yake Kristo tuna nguvu za kutuwezesha kuishi kwa njia inayofaa mbele zake Mungu. Nguvu na utukufu wote haumo ndani ya kiumbe kingine kile, bali umo ndani ya Mungu, kwa maana Yeye ndiye hutoa vipawa vyote vyema. Maombi haya yanaelekea kufikia tamati kwa imani, unyenyekevu, kumsujudu, na kumwabudu Yeye ambaye ndiye muumbaji.

“Hata milele.”—Muda usio na mwisho. Ufalme wa Mungu, rehema zake, na upendo wake ni mambo hayana mwisho.

“Amina.”—Kukubali. Iwe hivyo.

Maombi ndilo jambo muhimu zaidi katika uhusiano wetu na Mungu: Yesu alitupatia mwelekeo wa kuomba inavyokubalika mbele zake Baba, kwa maombi ya muda wa chini ya sekunde 30. Ombi hili silo ndefu na si la kuchosha bali ni matamshi ya moyoni, matamshi ya upendo, ya kumwabudu Mungu, huku tukisali kwa ajili ya mahitaji ya kila siku. Ombi hili la nguvu liko tofauti kabisa na maombi mengi ambayo hayana maana na ya kiburi ambayo huombwa manyumbani na katika makusanyiko ya makanisa ulimwenguni. Maombi ndio hutuunganisha na Mungu na ni muhimu kabisa maishani mwa Mkristo. Ombi la Bwana linaweza kuombwa kama lilivyoandikwa Maandikoni, mradi limeombwa kwa moyo mkunjufu. Zaidi, sehemu za ombi hayo zaweza kuunganishwa na maombi yetu ya kila siku tunayomwomba Baba yetu wa Mbinguni. Bwana, tufundishe kuomba . . . ■

Gazeti la *Ukweli wa Injili* ni jalida ambalo linatolewa kila robo ya mwaka kwa manufaa ya Kanisa la Mungu kwa ajili ya mafundisho na kwa ajili ya kuwahimiza Wakristo ili washike kweli za Biblia. Tutembelee katika tovuti yetu ya www.thegospeltruth.org na ujiandikishe ili uwe ukitumiwa notisi kwa njia ya barua pepe kila wakati jalida hili likiwa tayari ili uweze kupata toleo la kila kipindi. Gazeti hili la *Ukweli wa Injili* linachapishwa katika nchi nyingi ili lisambazwe katika nchi hizo. Kazi hii inawezekana kupitia kwa matoleo yanayotolewa kwa hiari. Pia wewe ukitaka unaweza kutumiwa risiti ya vile tumelipa ushuru kutokana na zawadi yako.

—Mhariri, Michael Smith

Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@the gospeltruth.org

Tahariri



Msijisumbue kwa neno lo lote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. — Wafilipi 4:6

Mpelekee Bwana maombini. Maombi hubadilisha hali. Omba mpaka upate jibu. Maombi ndio ufunguo. Nyimbo zinazotumia maneno hayo na matamshi hayo ndizo zinabunjika moyoni mwangu ninapojifunza somo la robo hii ya mwaka: maombi. Mara nyingi Wakristo huona kwamba maombi ni jambo ngumu na pia ni jambo la kuhukumu dhamira zao, kwa sababu wakati mwingi sisi hupuuza maombi. Lakini ni ombi letu kwamba Roho wa Mungu atatusaidia kuelewa kwamba maombi ni mweke na nafasi muhimu ya sisi kuweza kufanywa upya kwa njia ya upendo wake Mungu na Roho wake. Huu ni wakati bora wa kumwabudu Mungu, na pia ni wakati wa sisi kumtwika Bwana mizigo yetu. Je, ni jambo la baraka kubwa kiasi gani kwetu sisi kuweza kuyapeleka mambo yote mazito yaliyo mioyoni mwetu kwake Mungu, yule ambaye anatupenda na ambaye yu tayari kutusaidia kubeba mizigo yetu.



Tutembelee

www.thegospeltruth.org

ili kujiandikisha na

kupata jarida

za mbele.

Kuna nguvu nyingi zinazopatikana kutokana na maombi wakati tunamwendea Mungu kwa imani. Mimi mwenyewe nishapitia ujuzi wa kupata miujiza ya uponyaji, kutoa pepo, na hata kuwa na amani moyoni katika nyakati za shida; na mengi zaidi kupitia kwa nguvu za maombi. Zaidi ya hayo mimi nimeweza kufanya maombi hata wakati kunaonekana hakuna jambo linalobadilika; kwa maana ni wakati kama huo ndio imani yetu inahitaji kukita mizizi katika hekima yake Mungu, na sio kutokana na jibu ambalo tunalitarajia. Maombi hutubadilisha kwa maana yanatufikisha mahali pa kuwa watu wanaomtegea na wenye subira mbele zake Mungu. Ni wakati kama huo ambapo Mungu anaweza kufanya kazi yake kwa njia ya kuleta manufaa kwetu, kwa maana nguvu za maombi hazitokani na kile tunachofanya bali katika kile ambacho Mungu anatutendea kwa wema na rehema zake.

Lakini maombi silo jambo la mtu kufuata maagizo fulani ya jinsi ya kufanya maombi hayo, na pia maombi sio njia kamili ya sisi kuweza kuelezea maswala yote ambayo yanatukabili. Maombi ni zaidi ya mafundisho ya kidini, na kwa kweli ni njia ya mtu kujieleza kibinafsi, na kuwa na wakati wa kuwasiliana na Bwana na Mwokozi wake. Ni tumaini langu kwamba katika swala la maombi sisi hatutatumbukia kwenye lindi la mafundisho ya kidini. Hata ingawa mafundisho ya kidini ni muhimu, ni muhimu zaidi (sisi) kutambua baraka inayoletwa na maombi. Mimi nilistajabu sana niliposoma na kufanya utafiti katika maandiko mengi yanayohusiana na maombi. Basi toleo hili ni kionjo tu ya yale ambayo Biblia imefundisha, na kwa kweli haya sio mafundisho makamilifu kuhusiana na swala la maombi. Ombi langu ni kwamba kila msomi atapata himizo ya kutafuta mahali pasipo na kelele ambapo ataweza kuwasiliana na Bwana wake kwa njia ya maombi ambayo hayakomi maishani mwake. Utapata kwamba ukifanya hivyo jambo hilo litazidisha ukuaji wako kwa mambo ya kiroho, na pia litakuwa suluhisho la mambo mengi yanayokukabili, shida za ndoa, misukosuko ya kikanisa, nk; utapata kwamba maombi hayo yanakubadilisha kwa njia ya neema yake Mungu. Basi hebu tufanye maombi huku tukiwa na matarajio ya kupata mema.

Michael W. Smith

Januari 2020.

Kuomba Wakati wa Chakula



Mara nyingi katika Maandiko tunamwona Yesu akiomba kabla ya kula. “Akatazama juu mbinguni, akabariki, akaimega ile mikate, akawapa wanafunzi” (Mathayo 14:19). Katika maandiko tofauti tofauti waandishi wa Injili walitumia neno “kubariki,” ilhali wengine walitumia neno “kushukuru.” Ni jambo muhimu kuzingatia kwamba huenda katika jambo hili Yesu alikuwa akifuata tamaduni ya Wayahudi, ambayo haikuwa ya kubariki chakula, bali ya kumshukuru Mungu kwa ajili ya chakula hicho. Wayahudi walikatazwa kula wala kunywa kabla ya mtu kumtambua Mungu ambaye amempatia chakula hicho, kwa njia ya kumshukuru.

Baraka hiyo ambayo Wayahudi walisema ilitumia maneno yafuatayo: “Umebarikiwa ewe Bwana Mungu wetu ambaye pia ni Mfalme wa ulimwengu na ambaye ndiye hutubariki na chakula kutoka kwa udongo.” Basi tamaduni na mfano waliofuata haukuwa wa “kukibariki” chakula bali ilikuwa ni kumshukuru au kumbariki Mungu ambaye ndiye huwapatia watu wake chakula. Mtume Paulo “akatwaa mkate, akamshukuru Mungu mbele yao wote akaumegea akaanza kula” (Matendo 27:35). Tabia hiyo ya kumshukuru Mungu wakati wa mlo ni tabia nzuri ambayo inastahili kuigwa na watu wa Mungu, iwe ni chakula kinacholiwa hadharani, au chakula cha mtu akiwe peke yake. ■

Mwongozo wa Kujifunza Biblia

Somo: MAOMBI



Somo la Maandiko: *Ombeni bila kukoma.* —1 Wathesalonike 5:17

Maana: Maombi ni mtu kuwawasiliana na kufanya ushirika na Mungu. Ni tendo ambalo linahusisha “kutukuza, au kutamka maneno kueleza jinsi tunahisi kwamba Mungu ni mtakatifu, kukiri dhambi zetu, kuomba rehema na msamaha wake, kuwaombea watu wale wengine ili wapate baraka zake, na kutoa shukrani zetu” (*Kamusi ya Webster, 1828*).

Muhstasari: Maombi ndilo jambo la kipekee ambalo kupitia kwake wanadamu wanaweza kujua na kuwa na ushirika na Mungu. Ni njia ambayo kupitia kwake tunaweza kumwabudu na kumtukua Mungu. Hii ndiyo barabara ambayo inamwezesha mwanadamu kupata wokovu na neema za Roho wa Mungu. Kwa kweli maombi ni kamba inayounganisha Mbingu na Dunia na ambayo humwezesha mwanadamu kujua na kuelewa mapenzi yake Mungu. Maombi hubadilisha moyo wa mwanadamu kwa njia ya imani, na pia inaweza kubadilisha hali ambazo zinamkabili mwanadamu kupitia kwa nguvu zake Mungu. Kusema kweli maombi ni moja ya mambo muhimu zaidi yanayotuwezesha kuishi maisha ya Kikristo yenye ushindi.

I. Amri ya Kuomba

- A. “Imewapasa kumwomba Mungu sikuzote.” Luka 18:1.
- B. “Dumuni sana katika kuomba.” Wakolosai 4:2.
- C. Ombeni, tafuteni, bisheni Luka 11:9-10.

II. Kusudi/Umuhimu/Nguvu za Maombi

- A. Uhusiano/Ushirika. Mwanzo 5:24; Yeremia 29:11-13; Yohana 15:5.
- B. Ibada. Zaburi 103:1.
- C. Wokovu. Matendo 2:21.
- D. Uponyaji. Yakobo 5:13-16.
- E. Neema/Nguvu. Waebrania 4:16.
- F. Hekima. Yakobo 1:5.
- G. Kumwachia mizigo yetu. 1 Petro 5:6-7; Zaburi 107:28-30.
- H. Nguvu za kushinda. Mathayo 26:41.

III. Jinsi ya Kuomba

- A. Kwa jina la Yesu. Yohana 16:23.
- B. Kwa Imani. Waebrania 11:6
- C. Kwa unyenyekevu. Yakobo 4:6.
- D. Kwa Roho. Yuda 1:20.
- E. Kwa shukrani. Wafilipi 4:6.
- F. Kwa kutojirudiarudia. Mathayo 6:7-8.

IV. Watu Ambao Mungu Husikia na Kujibu Maombi Yao

- A. Walio wanyenyekevu/wenye kufanya toba 2 Mambo ya Nyakati 7:14
- B. Wenye kuhitaji ukombozi. Yoeli 2:32; Zaburi 86:7.
- C. Watakatifu na watiifu. Yakobo 5:16; 1 Petro 3:12; 1 Yohana 3:22.
- D. Wenye kuamini. Waebrania 11:6; Marko 11:24
- E. Kulingana na mapenzi yake. 1 Yohana 5:14-15.
- F. Kuomba kwa Roho. Warumi 8:26-27.

V. Vikundi vya Watu Wanaohitaji Kuombewa

- A. Sisi binafsi. Zaburi 55:16; 2 Wakorintho 12:8-10.
- B. Watakatifu/Wahudumu wa Injili. 1 Wathesalonike 1:2; Waefeso 6:18-19; 2 Wathesalonike 3:1
- C. Wafanyi kazi . . . wavunaji. Luka 10:2
- D. Wale ambao hawajaokoka. Warumi 10:1
- E. Maadui. Mathayo 5:44.
- F. Mataifa/Viongozi. 1 Timotheo 2:1-3

VI. Vizuizi vya Maombi

- A. Dhambi. Mithali 15:29; Yohana 9:31.
- B. Kuomba kwa nia mbaya. Yakobo 4:3.
- C. Kutosamehe. Marko 11:25-26.
- D. Utakatifu wa kibinafsi. Luka 18:9-14.
- E. Shida za ki-ndoa. 1 Petro 3:7.

VII. Mahali pa Kufanyia Maombi

- A. Mtu akiwa peke yake/mahali pa siri. Mathayo 6:5-6; Mathayo 14:23.
- B. Hadharani. Matendo 4:31; Matendo 12:5,12.

VIII. Ahadi kwa Waombaji

- A. “Mtapewa.” Mathayo 7:7-8
- B. “Kupatana/kukubaliana.” Mathayo 18:19
- C. “Ombeni mtakalo.” Yohana 15:7.

Tamati

Lakini mwisho wa mambo yote umekaribia; basi, iweni na akili, mkesho katika sala. —1 Petro 4:7

Mafunzo Kuhusu Maombi

MWITO WA KUNENA NA MUUMBAJI WETU

Maombi ni jambo la pekee linalodhihirisha uhusiano kati ya mtu na Mungu wake. Pia ni mweke mkubwa wa mtu kuingia kwenye uwepo wa Mungu na kuwasiliana naye—wakati wowote ule, mahali popote pale, na katika hali zozote zile. Maombi silo jambo la kufanywa tu mtu anapoitisha kile anachohitaji, bali ni wakati mwafaka wa kuabudu na kufanywa upya rohani.

Ni Jambo Lililofundishwa na Kristo

Yesu aliwafunza wanadamu “Imewapasa kumwomba Mungu sikuzote, wala wasikate tamaa” (Luka 18:1). Jambo hili limekaririwa katika Maandiko: “Dumuni sana katika kuomba, mkikeshwa katika kuomba” (Wakolosai 4:2). Mungu ana shauku la kuwa na uhusiano wa kibinafsi na wa karibu na mwanadamu. Lakini uhusiano

wa kuridhisha huchukua muda na unahitaji kutiliwa nguvu. Maombi ndio njia ambayo mwanadamu anaweza kutangamana na Mungu. Wakati hamna mawasiliano, basi hakutakuweco na uhusiano wenye maana. Ni mapenzi ya Mungu kwamba tutembe naye kila siku, kama Henoko alivyotembea naye. Yesu aliwarai wanafunzi wake kudumu ndani yake, kama tawi lidumavyo katika mzabibu. Maombi ni kipengee muhimu cha mtu kudumu ndani mwake Kristo, jambo lilalomwezesha mtu kushiriki mfano wa Kristo, na hata kuzaa matunda ya kiroho. Yakobo 4:8 inatwambia, “Mkaribieni Mungu, naye atawakaribia ninyi.”

Ibada ya Kweli Toka Moyoni

Maombi ya kweli yanahusisha zaidi ya mtu kunakili kitu ambacho kimeandikwa. Maana halisi ya maombi ni mtu kumtafuta Mungu kwa moyo

wake wote na pia kumkaribia Mwokozi: “Nanyi mtaniita, mtakwenda na kuniomba, nami nitawasikiliza. Nanyi mtanitifuta na kuniona, mtakaponitifuta kwa moyo wenu wote” (Yeremia 29:12-13). Wakati wa maombi ni wakati wa kumwabudu Bwana na kilitukuza jina lake. Maombi ndilo jambo ambalo huweka moyo na akili za mwanadamu katika hali nzuri ya kupokea kutoka kwa Mungu, na pia ndio humkumbusha mtu kuwa mtiifu.

Ni Funguo za Kufungua Milango

Umuhimu na nguvu za maombi si jambo linalostahili kuchukuliwa kwa urahisi, kwa maana maombi ya kweli ni ufunguo wa kufungua milango mingi. Maombi kutoka moyoni ndio huiletea nafsi ya mwanadamu wokovu. “Na itakuwa kila atakayeliitia jina la Bwana ataokolewa” (Matendo 2:21). Maombi ndio humwita Mungu kutoka kiti chake cha enzi ili aigilie kati kwa nguvu zake za Kiungu kwenye mtiririko wa wa mambo ya dunia ili mgonjwa apate uponyaji. “Mtu wa kwenu amekuwa hawezi? Na awaite wazee wa kanisa; nao wamwombe, na kumpaka mafuta kwa jina la Bwana. Na kule kuomba kwa imani kutamwoko mgonjwa yule, na Bwana atamwinua” (Yakobo 5:14-15). Katika Maandiko maombi yalibadilisha mambo mengi na hata sasa yanaendelea kufanya hivyo kwa manufaa ya watu wa Mungu katika kizazi hiki.


Njooi Kwangu

Katika shida na matatizo yetu maishani na masumbuko ya kiakili wito tunaopata kutoka kwa Mungu ni kuja kwake kwa uhakika: “Basi na tukikaribia kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji” (Waebrania 4:16). Ni kupitia ombi hilo la kujifungua peupe ndipo roho zetu zinamwagiwa neema yake. Basi sisi hukosa kiwango gani cha neema na amani kwa kukosa kutumia muda wetu maombini? Maombi ni mahali pa kumwaga yote yanayotusumbua na kuyaleta kwa Mwokozi ili tupate kitulizo (1 Petro 5:6-7). Zaburi 107:28-30 inatumia mchoro wa ajabu kufafanua swala hili: “Wakamlilia BWANA katika dhiki zao, akawaponya na shida zao. Huituliza dhoruba, ikawa shwari, mawimbi yake yakanyamaza. Ndipo walipofurahi kwa kuwa yametulia. Naye huwaleta mpaka bandari waliyoitamani.”

Mawasiliano ya Pande Mbili

Maombi si mawasiliano ya pande moja bali ni wakati wa mtu kuwa na utulivu uweponi mwake Mungu; ni mahali ambapo moyo wa mwanadamu humsikiliza Roho wake Bwana, ukitafakari kuhusu wema wake. Wakati wa maombi ndio ambao humpatia Mkristo nguvu za kukabiliana na maswala ya kila siku kwa nguvu zake Mungu. Hata utafiti wa kidunia umeonyesha

(Endelea katika Ukurasa 6)



“Maombi ni kipengele muhimu cha mtu kudumu ndani mwake Kristo, kitu cha kumwezesha mtu kushiriki mfano wa Kristo, na hata kumwezesha kuzaa matunda ya kiroho.”

kwamba maombi hupunguza masumbufu ya kiakili na wasiwasi wa mtu, na pia ni jambo linalomwezesha mtu kuwa na mwelekeo bora wa kiakili maishani.

Maombi ni nafasi ya mtu kumtafuta Mungu ili kupata uongozi na hekima (Yakobo 1:5). Ndiposa tunaambiwa: “Kesheni, mwombe, msije mkaingia majaribuni” (Mathayo 26:41). Maombi ni chanzo cha nguvu ya kushinda mitego na majaribu ya adui.

Jinsi ya Kuomba

Kulingana na yaliyoandikwa katika Biblia, na pia kwa mifano iliyomo, twaweza kujifunza njia bora ya kuomba. Wakristo wanastahili kuomba kwa jina la Yesu (Yohana 16:23). Kuna nguvu katika jina la Yesu ndiposa tunastahili



kuomba kwa jina hilo kwa heshima na pia kwa mamlaka. Watu binafsi wanastahili kumtafuta Mungu kwa imani, wakiamini kwamba Yeye “huwapa thawabu wale wamtafuta” (Waebrania 11:6). Maombi yanayokubalika ni yale hufanywa kwa unyenyekevu wa moyo na roho (Yakobo 4:6), bila kiburi na utakatifu wa kibinafsi. Tunahitaji kumwenda Bwana kwa mahitaji yetu huku tukimpa

shukrani (Wafilipi 4:6) na asante. Yesu aliwafundisha wafuasi wake kuomba kwa urahisi bila “kupayuka-payuka” (Mathayo 6:7-8) kwani Yeye ajua mahitaji yetu hata kabla ya sisi kufanya maombi hayo. Kamwe maombi hayastahili kutamkwa ili watu wakushangae au kujionyesha, bali kwa ajili ya kupatana na Mungu katika Roho. Ni jambo la baraka kuu kujua kwamba hata kama maneno na mawazo hayaelezeki kwa uwazi, kutokana na mtu kuwa na uzito wa moyo na kujisikia kwamba hana nguvu, Roho wa Mungu “hutuomba kwa kuugua kusikoweza kutamkwa” (Warumi 8:26-27).

Mtu Ambaye Bwana Humsikia

Mahali kwingi katika Biblia tumeonyeshwa kwamba Mungu hutega sikio lake na kujibu maombi ya watu wakati wametimiza matakwa fulani. Yeye hujibu maombi ya mtu mnyenyekevu mwenye roho ya toba (2 Mambo ya Nyakati 7:14). Pia Yeye hujibu maombi ya wanaomwita wakati wanahitaji ukombozi (Yoeli 2:32). “Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii” (Yakobo 5:16). Yeye anaheshimu maombi ya watakatifu na wale wanaotii amri zake (1 Yohana 3:22). Kutoka kwenye kiti chake cha enzi Yeye huinuka na mambo yakabadilika wakati maombi yanapofanywa kwa imani (Marko 11:24), yanapofanywa kulingana na mapenzi yake (1 Yohana 5:14-15).

Maombi Yafanyayo Kazi Yake

Kuna mambo ambayo yatazuia maombi kufaulu. Yohana 9:31: “Twajua ya kuwa Mungu hawasikii wenye dhambi.” Mayo Mithali 15:29 yasema, “BWANA yu mbali na wasio haki; bali huisikia sala ya mwenye haki.” Mungu ni mtawala mkuu na hatajibu kila ombi, hasa ombi linaloombwa kwa njia ambayo haifai ili mtu atumie anachopata kwa tamaa zake (Yakobo 4:3). Roho ya kutowasamehe wale wengine (Marko 11:25-26), au ya

utakatifu wa kibinafsi (Luka 18:9-14) pia itakuwa ni kizuizi kwa maombi. Shida za ndoa, ukosefu wa neema ya mmoja kwa mwingine pale nyumbani ni mambo ambayo yatakuwa kizuizi kikuu kwa kazi ya maombi. “Ninyi waume, kaeni . . . na kumpa mke heshima . . . kusudi kuomba kwenu kusizuiliwe” (1 Petro 3:7).

Mambo Tunayopaswa Kuomba

Kuna watu tofauti na mambo tofauti ambayo Biblia inatufundisha kuomba. Baada ya ibada na shukrani zako ni jambo linalofaa mtu kujiombea: maombi kuhusu kukua kiroho, kupata nguvu za kiroho, na pia kupata nguvu za kihisia, na hata mahitaji ya kila siku. Omba kwa ajili ya familia yako, mahitaji ya watu wale wengine, ombea wale hawajaokoka, na uombee maadui zako, waombee watakatifu na wahudumu wa injili, ili Bwana atume wafanyi kazi; ombea mataifa na viongozi wote, kwa sababu maombi kama hayo yanalingana na maandiko na makusudi bora ya maombi.

Maombi ya Kibinafsi na ya Kufanywa Hadharani

Biblia inaonyesha kwamba kuna wakati wa maombi ya kibinafsi na pia kuna wakati wa maombi ya hadharani. Mwanzoni wa huduma Yesu alihitaji nguvu kutoka kwa Baba yake, na wakati mwingi alijitenga kuomba. Kuna rekodi nyingi kwenye Biblia za watu wa Mungu wakiomba kwa umoja mbele zake Baba kwa ajili ya mahitaji maalum. Kuna nguvu katika maombi yenye umoja, maombi hayo huinuka kama manukato na kufika kwenye kiti cha enzi cha Mungu. Wakati wa maombi ya kibinafsi ni wakati wa mtu kutoa mambo yote ndani mwake mbele zake Mungu. Lakini kwenye maombi ya hadharani mwombaji anahitaji kuwapa wasikilizaji wake heshimu kwa yale anayoombea, na hata kwa muda anaotumia kufanya maombi hayo.

Wakati Unaofaa Kuomba

Katika historia Wayahudi walikuwa na nyakati mbili za maombi—asubuhi na usiku; lakini wanahistoria wengine huongezea wakati wa tatu, saa sita mchana. Danieli aliomba mara tatu kwa siku (Danieli 6:10). Lakini Agano Jipya halijafundisha kuhusu nyakati maalum za maombi, bali linafundisha kwamba “tuombe bila kukoma” (1 Wathesalonike 5:17). Mtoto wa Mungu anahitaji kuwa na roho ya maombi, maombi ambayo hayakomi. Lakini pia ni muhimu kuwa na wakati maalum wa kuomba na kumtafuta Bwana. Huenda ikawa wakati unaofaa zaidi kufanya maombi ni ule wa asubuhi, kabla ya mtu kupambana na siku yake, na baadaye hapo jioni, wakati siku yake inafika kikomo. Maisha ya kiroho hupata nguvu kwa mtu kuwa na wakati mwingi na wenye mpango wa kufanya maombi na kujitoa kwa Mungu.

Kukeshwa na Kuomba

Maombi ni mtu kukutana na Mungu wake na kusudi kuu la kuomba si mtu kupata majibu ambayo hayadumu milele, bali ni mweke wa mawazo na roho zetu kubadilishwa na Mungu. Nguvu na manufaa makubwa hupatikana kutokana na maombi. Na kwa maneno ya mtume Petro, “Mwisho wa mambo yote umekaribia; basi, iweni na akili, mkeshe katika sala.” ■



Je, mtu anahitaji kuwa amesimama au kukaa vipi anapofanya maombi yake?

Hakuna njia moja inayofaa ambayo mtu anastahili kuwa amesimama au kukaa anapofanya maombi yake. Kati ya Wayahudi, kabla ya wakati wa Kristo, wakati mwingi watu walifanya maombi huku wakiwa wamesimama. Inaonekana kama kwamba Hana alikuwa amesimama hekaluni alipofanya maombi ya kumpata mtoto Samueli (1 Samueli 1:26). Yesu naye akasema hivi, “Nanyi, kila msimamapo na kusali, sameheni . . .” (Marko 11:25).

Kupiga magoti wakati wa kufanya maombi ni jambo ambalo kwa kawaida lilifanyika wakati watu walikuwa wakifanya maombi au sherehe maalum, hata ingawa tunasoma kwamba nabii Danieli aliomba mara tatu kwa siku, huku akiwa amepiga magoti (Danieli 6:10). Mfalme Sulemani alipiga magoti wakati hekalu lilikuwa likiwekwa wakfu (1 Mfalme 8:54). Naye Ezra alipiga magoti mbele zake Mungu alipokuwa akifanya maombi kwa moyo mzito (Ezra 9:5). Daudi naye akasema, “Njooi, tuabudu, tusujudu, Tupige magoti mbele za BWANA aliyetuumba” (Zaburi 95:6). Na katika Maandiko ya Mitume 21:5 kuna rekodi ya watakatifu wa Agano Jipya wakipiga magoti. Naye Mtume Paulo anaonekana akipiga magoti katika Matendo 20:36.

Katika Agano la Kale kumenakiliwa matukio mengi ya watu wakilala kifudufudi huku vichwa vyao vikiguza sakafu wakati watu wa Mungu walipokumbana na majanga makubwa na majonzi. Nabii Eliya aliomba huku akiwa amelala sakafuni na uso wake ukiwa katikati ya miguu yake (1 Wafalme 18:42). Na katika nyakati za Ezra watu walimwabudu Mungu huku nyuso zao zikiguza ardhi (Nehemia 8:6).

Kulingana na Maandiko kuna njia tofauti za kufanya maombi, na itakuwa ni mawazo ya kibinadamu ikiwa watu wataunda sheria kuhusu njia moja inayofaa ya kufanya maombi. Wakati wetu wa maombi unastahili kuwa wakati wa kumheshimu Mungu kwa kufanya maombi kwa njia ambayo inamtukuza na kumwabudu Yeye. Ni baraka kubwa mtu kufanya maombi akitembea, akiendesha gari, akiwa amelala chali – lakini pia ni jambo muhimu mtoto wa Mungu asiwe mvivu na kuachana na njia inayofaa ya kufanya maombi, njia ya kawaida, na njia yenye unyamavu wa kumsikiliza Bwana.

Ni jambo muhimu kutambua kwamba Agano Jipya linatufundisha “wanaume wasalishe kila mahali, huku wakiinua mikono iliyotakata” (1 Timotheo 2:8). Kuna mifano mingi ya kanisa la Agano la Kale washirika wake wakiomba huku wakiinua mikono yao kumpatia

Bwana sifa na kufanya sala kwa Bwana Mungu. Hata ingawa (pengine) hakuna haja ya Mkristo kuinua mikono kila wakati anapofanya maombi, mimi naonelea litakuwa jambo ambalo linalingana na Maandiko ikiwa watu watainua mikono wakati wanapofanya sifa maalum au maombi maalum kwa Bwana.

Je, Biblia Inafundisha Nini Kuhusu Lugha ya Kibinafsi ya Mtu Kufanya Maombi?

Ni muhimu kwetu kuongozwa na Biblia badala ya kuongozwa na ujuzi au mazoea ya wale wanaojiita Wakristo. Biblia haina mafundisho kuhusu lugha shesheli ya kuomba maombi ya kibinafsi, maanake kuomba kwa lugha ambayo haijulikani na mtu mwingine, lugha ya mbinguni. Je, tunahitaji kutumia mfano upi ambao ni bora zaidi wa kuomba kuliko ule ambao tuliachiwa na Kristo mwenyewe? Yesu alifundisha wanafunza wake kuomba kwa lugha ya kawaida kabisa na kwa urahisi wa lugha (Mathayo 6:19-23).

Mara nyingi watu wanaounga jambo hili mkono hunukuu 1 Wakorintho 14:14 “Maana nikiomba kwa lugha, roho yangu huomba, lakini akili zangu hazina matunda.” Lakini zingatia kwamba neno “isiyojulikana” ni neno ambalo liliongezwa na watafsiri wa Biblia, na maana ya “lugha” hapa ni glossa, ambalo maana yake halisi ni lugha ya kigeni. Basi hapa haikumaanisha mtu kutamka maneno yasiyoeleweka maombini. Kama mtu ataomba kwa lugha ya kigeni, ambayo mwenye kuomba mwenyewe anailewa, lakini hakuna mtu mwingine chumbani mle ambaye anailewa, basi kueleweka kwa ombi lake na wale wanaomsikiliza hakutakuwapo, na hakuna mtu atajengeka kutokana na ombi hilo. Mstari wa 15 unapeana maelezo zaidi kuhusiana na swala hilo: “Imekuwaje, basi? Nitaomba kwa roho, tena nitaomba kwa akili pia; nitaimba kwa roho, tena nitaimba kwa akili pia.”

Katika Mathayo 6:7 Yesu anafundisha kwamba tusitumie maneno ya kurudiarudia tunapofanya maombi kama wanavyofanya makafiri. Basi maombi yetu yanahitaji kuombwa kwa njia ya wazi na yenye kueleweka vizuri, na maombi hayo yawe yametokana na nia safi moyoni.

Mtu Anastahili Kuomba kwa Muda Gani?

Hamna kiwango ambacho kimewekwa cha muda ambao mtu anastahili kutumia maombini. Mfano huu wa Ombi la Bwana ulikuwa wa ombi ambalo halikutumia sekunde 30. Wakati mwingine Yesu aliomba usiku kucha ilhali mara nyingine aliomba kwa muda mfupi. Kwa upande mmoja baadhi ya watu hawaombi vya kutosha, ilhali wengine wamo utumwani na wanaweza kutumia masaa mengi kila siku maombini huku wakipuuza majukumu yale mengine. Lakini hali ya wakati uliopo ndiyo ambayo inastahili kuongoza ni muda gani mtu atatumia maombini. Wakati mtu amebeba mizigo mizito, maombi ya kibinafsi yanaweza kuchukua muda zadi au hata kuombwa usiku kucha. Wakati mwingine inambidi mtu kutumia wakati maombini ili kuweza kuingia katika roho ya kuomba. Kwa kawaida maombi ya hadharani sio wakati bora wa kuomba maombi marefu. Jambo ambalo ni muhimu zaidi ni sisi kuweza kupatana na Mungu na kuchukua muda maombini ili kuweza kumwabudu na kuleta maombi yetu kwake. Lakini ukweli ni kwamba watu wengi hawana shida hiyo ya kuomba sana!



JE, WAJUA?

Shanga za maombi hutumiwa na dini tofauti ulimwenguni, kama vile dini ya Kihindi, ya Butha, ya Kikristo, ya Kiislamu na ahata ya Kikalasinga kwa lengo la kurudiarudia maombi, kurudia matamshi ya kidini, na hata kwa ajili ya kuabudu. Hata ingawa haijulikani maombi ya kutumia shanga yalianza wapi, inaonekana kama kwamba shanga za maombi zilitumiwa kwenye ustarabu wa kipagani tangu karne thelathini na sita (36) zilizopita. Katika historia na rekodi zilizoko, dini ambayo ilitumia shanga kufanya maombi tangu zamani sana ni ile ya Kihindi.

Dini hiyo ilitumia shanga katika maombi mamia ya miaka kabla ya kuzaliwa kwa Kristo.

Yesu alifundisha wanafunzi wake kwamba wasiombe kama makafiri kwa kurudiarudia maombi. Maombi ni tendo la mtu kufungua moyo wake kwa Mungu, na sio tendo la kuweka maneno fulani akilini ambayo mtu anarudia-rudia. Matumizi ya shanga za ombi ni jambo ambalo halilingani na mafundisho ya Kristo.



OMBI LA YABESI

Huyo Yabesi akamlingana Mungu wa Israeli, akisema, Lau kwamba ungenibarikia kweli kweli, na kunizidishia hozi yangu, na mkono wako ungekuwa pamoja nami, nawe ungenilinda na uovu, ili usiwe kwa huzuni yangu! Naye Mungu akamjalia hayo aliyoyaomba.

— 1 Mambo ya Nyakati 4:10

Ombi la Yabesi ni mfano bora wa ombi fupi linaloheshimiwa na Mungu. Jambo la kwanza Yabesi aliomba ni Mungu kumbariki. Kusema kweli tunahitaji baraka za Mungu maishani mwetu, bila Yeye tutapotea njia na kukata tamaa. Mungu ndiye hutupatia pumzi na kila kipawa kizuri. Ni bora sisi kumtafuta ili awe msaada na nguvu zetu, badala ya kuweka tumaini katika uwezo wetu binafsi au kwa wenzetu. Watu wengine watahindwa kutusaidia, lakini Mungu ni wa kutegemewa, kwa maana Yeye habadiliki.

Panua mipaka yangu Bwana. Nisaidie kukua kiroho. Nipe nguvu na neema ya kukua. Nibariki na uwezo wa kushinda majaribu ninayopambana nayo. Angusha kuta ambazo zimekita mizizi maishani mwangu. Eneza mipaka ya maisha yangu ya kiroho niweze kushiriki Injili na wale ambao wako nje ya mipaka yangu.

Ee Bwana, naomba uwekelee mkono wako maishani mwangu? Mimi siwezi.

Nanyenyekea mbele ya kiti chako cha enzi kuomba kwa moyo wa dhati, ueneze rehema zako kwangu. Nahitaji uongozi wako maishani. Nahitaji hekima na uhuisho wako. Nina shauku kubwa kupata upako wako, kukubalika machoni pako.

Ee Bwana tuepushe maovu ili yasituangamize. Nisaidie kumsikiliza Roho Mtakatifu. Mimi sina utakatifu wa kibinafsi, nifungue macho yangu yenye upofu ili nione. Nionyeshe mitego ya adui. Nidumishe dhidi ya kupenda ulimwengu na dhidi ya hadaa za dini ambazo sio za kweli. Njia yako ndio ambayo huongoza mtu hadi Mbinguni. Naomba unipe usalama na ulinde nafsi yangu nisitende dhambi dhidi yako.

Mungu alisikia maombi ya Yabesi. Biblia inasema, "Mungu akamjalia hayo aliyoyaomba." Hivyo ndivyo Mungu atatutendea. Bwana apewe sifa! Mwenzangu, mtoto wa Mungu, kuwa mtu hodari mwenye ushujaa. Tuendelee kuomba! ■

Maombi Yanayojulikana Sana

OMBI LA BWANA
Mathayo 6:9-13

OMBI LA YONA LA KUOKOLEWA
Yona 2:2-9

OMBI LA HEZEKIA AKIOMBEA UPONYAJI
2 Wafalme 20:1-5

OMBI LA SULEMANI LA KUWEKA HEKALU WAKFU
1 Wafalme 8:22-53

KUHANI MKUU YOSHUA
Nehemia 9:5-38

OMBI LA YABESI
1 Mambo ya Nyakati 4:10

Anwani

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA

Email:
editor@thegospeltruth.org

UTAKATIFU KWA BWANA